

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN AFUNGUA MRADI WA MABASI YAENDAYO HARAKA, AWAMU YA PILI (BRT II) DAR ES SALAAM



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dk Sidi Ould Tah ndani ya basi liendalo haraka wakielekea Mtoni kwa Aziz Ally, kufungua Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka, Awamu ya Pili (BRT II) unaohusisha Barabara ya Kilwa, Chang'ombe, Sokoine na Kawawa, Dar es Salaam jana. Kushoto ni Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega.



Rais Samia na Rais wa AfDB, Dk Tah wakizindua Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka, Awamu ya Pili (BRT II).

Rais Samia akikata utepe kuzindua huduma ya mabasi yaendayo haraka katika Barabara ya Kilwa, Chang'ombe, Sokoine na Kawawa.



Rais Samia na Rais AfDB, Dk Tah wakizungumza na dereva wa basi liendalo haraka, Happiness Aloyce baada ya kufika katika Kituo cha Mbagala Rangitatu.



Rais Samia akihutubia viongozi, wageni na wananchi wa Mtoni kwa Aziz Ally baada ya kuzindua Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili (BRT II).



Wakazi wa Dar es Salaam wakiwa kwenye hafla ya uzinduzi wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili (BRT II). (Picha zote na Ikulu).

KONA YA JAMII 9

MWANANCHI.CO.TZ

Madereva mheshimu uhai wa abiria

Kila ajali ukifuatilia taarifa ya polisi unaona uzembe ulikuwa wa dereva kulipita basi au malori bila tahadhari, wewe dereva kwa nini huheshimu uhai wa abiria wako?

Semme

Ajali ya Isamilo na Libanike taarifa ya awali ya polisi inasema kuna uzembe wa dereva. Watu wanapoteza maisha lakini inabaki tu historia. Madereva zingatieni usalama wa abiria waende na warudi salama.

Agnes

Biashara zinazotumia mashine nzito zimeanza kuanzishwa katikati ya makazi bila kuzingatia athari za kelele. Wananchi wengi hukosa utulivu wa kupumzika au kusoma kutokana na kelele hizo.

Emma Mzalendo

Miji mingi inaendelea kujengwa bila kupanda miti ya kutosha. Kutokana na hali hiyo, joto huongezeka na wananchi hukosa maeneo yenye kivuli wanapokuwa wakisubiri huduma mbalimbali.

Rehema Luwa

Vitabu na magazeti mengi huishia kutupwa dampo badala ya kutolewa kwa shule au maktaba, hii inachangiwa na kukosekana kwa vituo vya kukusanya vitabu kunapunguza fursa za watoto kupata vifaa vya kujifunzia.

Mwinuka Hassanali

Baadhi ya taasisi hufungua ofisi kwa kuchelewa licha ya kutangaza muda rasmi wa kazi. Wananchi hulazimika

kusubiri kwa muda mrefu na kupoteza muda wa kufanya shughuli nyingine.

Salim Rahman

Watu wengi wanaokota simu au nyaraka muhimu hushindwa kujua namna sahihi ya kuzirudisha kwa wamiliki jambo lililochangiwa na kukosekana kwa mfumo rahisi wa kurejesha mali zilizookotwa na hivyo kunawaongezea wananchi hasara.

Lyn Mmasi

Katika baadhi ya maeneo, vibao vya majina ya mitaa vimeharibika au kuondolewa. Hali hii huwapa shida wageni, wahudumu wa dharura na kampuni za usafirishaji kufika maeneo husika.

Faraja Mushi

Maktaba na maeneo ya kusomea kwa utulivu yamepungua katika miji mingi hivyo vijana hulazimika kusomea kwenye mazingira yenye kelele yanayopunguza umakini.

Malisa Mkubwa

Saa za umma zilizokuwa katika baadhi ya maeneo zimepotea. Wananchi wengi, hasa wasiokuwa na simu, hukosa njia rahisi ya kufahamu muda.

Dorcus Mwakipele

Chemchemi nyingi za asili zimeharibiwa na shughuli za kibinadamu bila kulindwa. Hali hiyo hupunguza vyanzo vya maji kwa jamii zinazovitegemea.

Ritha Kimaro

Ofisi nyingi hazina sanduku

la maoni linalofanya kazi ipasavyo jambo linalofanya wananchi hukosa nafasi ya kutoa mapendekezo au malalamiko kwa njia salama.

Mfaume Kamani

Njia nyingi za waenda kwa miguu zimegeuzwa sehemu za biashara au maegesho ya magari. Hali hii huwalazimu watembea kwa miguu kutumia barabara kuu na kuhatarisha maisha yao.

Anne Mruma

Wananchi wengi hawazifahamu namba za huduma za dharura kama zimamoto au ambulansi. Elimu ndogo kuhusu huduma hizi huchelewesha uokoaji wakati wa majanga. Naomi Mushi

Salma

Waendesha baiskeli hukosa maeneo rasmi ya kupata huduma ndogo za haraka kama kujaza upepo au kurekebisha tairi. Hii huathiri matumizi ya usafiri huo rafiki kwa mazingira.

Lisa Mgheni

Vibao vya tahadhari katika maeneo ya ujenzi au barabarani mara nyingi huachwa vikiwa vimeharibika. Hali hii huongeza uwezekano wa ajali kwa watumiaji wa maeneo hayo.

Gire Ellud

Katika vituo vikubwa vya usafiri na maeneo ya huduma za umma, sehemu salama za kuchaji simu ni chache. Wananchi hulazimika kutumia huduma zisizo salama au kubaki bila mawasiliano wakati wa dharura.

Hajira Matiko

Baadhi ya watoa huduma hawabandiki orodha za bei katika maeneo yao ya biashara. Hali hiyo huwafanya wateja kutozwa gharama tofauti kwa huduma ileile na kuzua malalamiko yasiyo ya lazima.

Ibrahim Mganga

Licha ya kampeni za usafi, baadhi ya wananchi hutupa chupa, mifuko na taka ndogo kwenye mifereji ya maji. Taka hizo huziba njia za maji na kusababisha mafuriko hata wakati wa mvua zisizo kubwa.

Mfinanga

Mabomba ya maji yanapovuja kwa muda mrefu bila kutengenezwa husababisha upotevu mkubwa wa maji safi. Wananchi wanaosumbuliwa na uhaba wa maji huumia kuona rasilimali hiyo ikipotea bila hatua za haraka kuchukuliwa.

Alex Rutafungwa

Baadhi ya majengo na maeneo yenye historia muhimu kwa jamii huachwa yakiharibika bila kutunzwa, matokeo yake ni kupotea kwa kumbukumbu muhimu ambazo zingesainia vizazi vijavyo.

Happy Mlay

Katika baadhi ya vijiji na pembezoni mwa miji, madaraja madogo yanayotumiwa na wananchi kuvuka mifereji au mito yamechakaa kwa muda mrefu.

Rose Komba